KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 22, Issue 2

20th Jumaadal Aakhira 1433

11th MAY, 2012

HADEETH ZA MTUME (صلى الله عليه وسلم) ZINAZOKATAZA KUYAFANYA MAKABURI KUWA NI MISIKITI

NA: SHEIKH MUHAMMAD NAASIR-UD-DEEN AL-ALBAANI (رحمه الله)

HADEETH: Imepokewa kutoka kwa ‘Aaisha (رضي الله عنها) yakwamba amesema: Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم), *“Allaah na awalaani Mayahudi na Manaswara! Waliyafanya makaburi ya Mitume wao kuwa ni misikiti.’* Akasema ‘Aaisha, “Lau kama haingekuwa hivyo, basi kaburi lake (صلى الله عليه وسلم) lingelikuwa mahali palipo wazi, lakini alichelea yakwamba pangelifanywa kuwa ni mahali pa kufanya ‘Ibaada.”

MAELEZO: Kaburi lake (صلى الله عليه وسلم) lingelikuwa mahali palipo wazi, na wala lisingezungukwa na vizuizi vyovyote; na maana yake ni kwamba lingelikuwa nje ya nyumba yake. Haya yameelezwa katika *Fat-hul-Baari*.

NUKTA YA FAIDA: Maneno haya ya ‘Aaisha yanadhihirisha waziwazi sababu zilizowapelekea Maswahaba wamzike Mtume (صلى الله عليه وسلم) ndani ya nyumba yake — jambo lilokatiza kabisa njia kwa yoyote aliyekuwa [pengine] na lengo la kujenga msikiti juu yake. Kwa hali kama hiyo, imekuwa hairuhusiwi kuyachukulia hayo yaliyotangulia kuwa ni dalili ya kumzika mtu yoyote asiyekuwa yeye (صلى الله عليه وسلم) ndani ya nyumba yake. Jambo hili vilevile limetiliwa nguvu na ukweli yakwamba kufanya hivyo itakuwa ni kwenda kinyume cha msingi uliothubutu kuhusiana na mazishi, kwani Sunnah ni kwamba mazishi hutekelezwa kwenye makaburi. Kwa ajili hii, Ibn ‘Urwah amesema katika ‘*Al-Kawaakib ad-Daraari* (Uk. 77/*tafsir* 538), “Na mazishi kwenye makaburi ya Waislamu yalipendekeza zaidi kwa Abu Abdullaah (Imaam Ahmad) kuliko kuzikana majumbani, kwani kufanya hivyo madhara yake ni madogo kwa wenye kuendelea kuishi miongoni mwa waliofiwa, na hufanana zaidi na nyumba ya Akhera, na matokeo yake ni kupatikana kiwango kikubwa cha maombi (du’aa’) na kupatikana idadi kubwa ya watu watakaokuwa wakimuombea du’aa’. Na Maswahaba waliowafuata wao na wale waliokuja baada yao hawakuacha kuwazika watu kwenye majangwa. Kwahiyo, iwapo itasemwa, “Basi mbona Mtume (صلى الله عليه وسلم) amezikwa nyumbani mwake, na makaburi ya Maswahaba zake wawili vilevile yako hapo pamoja nae?”. “Sisi twasema”, akasema ’Aaisha, “Hilo limefanywa hivyo tu kwa sababu lisije kaburi lake likafanywa kuwa ni mahali pa kufanya ’Ibaada, na vilevile kwa sababu Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akiwazika Maswahaba zake katika makaburi ya Baqee’ - na kitendo cha Mtume (صلى الله عليه وسلم) hupewa kipaumbele kuliko vitendo vya wasiokuwa yeye [pamoja na ukweli yakwamba] Maswahaba zake wameonelea yakwamba jambo hilo lilikuwa ni lenye kumuhusu yeye peke yake, (صلى الله عليه وسلم), na kwa sababu imepokewa yakwamba, *“Mitume huzikwa mahali wanapokufia, na kuwalinda wao na makundi makubwa ya watu, na kuwatambua wao wakiwa miongoni mwa wasiokuwa Mitume.”*

Hadeeth nyengine kama hii ya ‘Aaisha pia imepokewa kutoka kwa babake (رضي الله عنهما). Amepokea Ibn Zanjawaih katika kitabu chake yakwamba ’Umar, mtumwa aliyeachwa huru wa Ghafrah amesema, “Walipokuwa wakijadiliana kuhusu mazishi ya Mtume (صلى الله عليه وسلم), mtu mmoja alisema, ‘Sisi tutamzika pale mahali alipokuwa akiswali!’ Basi Abu Bakr akasema, ’Mimi naomba hifadha kutoka kwa Allaah (Yaa Allaah tuepushe na hayo!) tusije tukamfanya awe ni sanamu wa kuabudiwa.’” Wengineo wakasema, “Sisi twaona bora tukamzike Baqee’, mahali ambapo ndugu zake miongoni mwa Muhaajir walipozikwa.” Akasema Abu Bakr, “Kwa hakika sisi hatupendi kuona yakwamba kaburi la Mtume wa Allaah (صلى الله عليه وسلم) likawe kwenye makaburi ya Baqee’ kisha watu [waanze] kuliabudu, jambo ambalo Allaah [Peke yake] ndiye anaestahiki, na haki ya Allaah ni zaidi ya haki ya Mtume wa Allaah. Na iwapo sisi tutavunja mkataba wa Allaah (katika maandishi asili imeandikwa: iwapo tutaichelewesha) tutasababisha haki ya Allaah kupotea. Kwahiyo, ikiwa tutavunja mkataba wa Allaah vilevile tutakuwa tumevunja mkataba kuhusu kaburi la Mtume wa Allaah (صلى الله عليه وسلم).” Wakasema, “Sasa hebu tueleze wewe Abu Bakr wafikiriaje?” Akasema, “Mimi nilimsikiya Mtume (صلى الله عليه وسلم) akisema, *“Allaah hajawahi hata mara moja kuichukuwa roho ya Mtume isipokuwa alizikwa palepale mahali ilipochukuliwa roho hiyo.”* Wakasema: “Kwahivyo, *Wallaahi*, umeridhika na kutushawishi nasi.” Kisha wakachora mstari ulozunguka kitanda chote, kisha ‘Ali, ‘Abbaas na al-Fadhl na jamaa zake wakamuinua na Maswahaba wakaanza kuchimba, wakachimba pale kilipokuwepo kitanda.”

HADEETH: Imepokewa na Abu Hurairah (رضي الله عنه) aliyesema: “Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم):

YALIYOMO

CHAKULA CHA MAITI 1

MIUJIZA YA MTUME 2 - 4

USIKOSE MAWAIDHA YA KUHUSU TAWHEED KATIKA MSIKITI WA MAZRUI KILA SIKU BAADA YA MAGHRIB MPAKA ‘ISHAA’. NA USTADH NA’MAN

"Allaah na awalaani Mayahudi! Wameyafanya makaburi ya Mitume wao kuwa ni sehemu za kufanya 'Ibaada."

HADEETH: Imepokewa kutoka kwa 'Aaisha na Ibn 'Abbaas (رضي الله عنهما) yakwamba alipokuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwenye kitanda chake cha mauti, alijiekea blangeti ya sufi juu ya uso wake, na pindi alipokuwa akisikiya joto na pumzi zake kupotea, aliliondoa na akasema,*"Laana ya Allaah iwe juu ya Mayahudi na Manaswara! Waliyafanya makaburi ya Mitume wao kuwa ni sehemu za kufanya 'Ibaada."* Akasema 'Aaisha, "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akiwaonya (Waislamu) wasifanye kama walivyokuwa wakifanya."

MAELEZO: Neno lililotumika kwenye riwaya hiyo lilikuwa ni '*Khameesah'* [خَمِيْصَةٌ] na limeelezwa maana yake kuwa ni hariri [*khazz*/خَز] au ya kitambara cha sufi, blangeti lenye michoro kama ilivyotajwa katika kitabu cha *an-Nihaayah*. Mimi [Sheikh al-Albaani] nasema: "Na lililokusudiwa hapa ni la pili, kwani *khazz* ni Hariri na ni maarufu na imeharamishwa kwa wanaume kama ilivyothubutu katika Sunnah, kinyume cha wenye kuihalalisha kwa miongoni mwa wanavyosema wale watu wasiotia uzito wowote katika Sunnah.

Amesema al-Haafidh Ibn Hajar, "Na ni kama kwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akijua kuwa ataondoka [hapa ulimwenguni] kutokana na maradhi hayo. Kwahiyo akahofia lisije kaburi lake likatukuzwa kama walivyofanya wale waliopita [katika makaburi ya Mitume yao], kwahiyo akawalaani Mayahudi na Manaswara, akiashiriya lawama [zake] kwa yoyote atakaefanya kama hivyo walivyofanya hao." Mimi nasema: "Kutokamana na Ummah huu na katika hadeethy nambari sita itakayofuata hapa ni tangazo la wazi lenye kuwakataza waona mambo hayo, kwahiyo kuwa na hadhari.

HADEETH: Imepokewa kutoka kwa 'Aaisha (رضي الله عنها): "Wakati wa maradhi [ya mwisho] ya Mtume (صلى الله عليه وسلم), baadhi ya wake zake walitaja kanisa moja nchini Ethiopia liitwalo Maariyah - na Umm-Salamah na Umm Habeebah walishawahi kwenda nchini Ethiopia - basi wakataja uzuri [wa kanisa hilo] na masanamu yaliyokuwemo ndani yake." Akasema, "[Basi Mtume (صلى الله عليه وسلم) akainua kichwa chake] akasema, '*Watu wale - anapokuwa mtu mwema miongoni mwao na akafa - hujenga mahali pa kuabudu [Masjid] juu ya kaburi lake na wakachora yale mapicha ndani yake. Wao ndio watakaokuwa watu waovu zaidi mbele ya Allaah [katika siku ya kufufuliwa]."*

Amesema al-Haafidh Ibn Hajar katika Fat -hul-Baari: Hadeeth hii ni dalili ya kuharamishwa kujenga misikiti juu ya makaburi ya watu wema, na kuchora picha zao ndani yake kama walivyokuwa wakifanya Manaswara. Na hapana shaka yakwamba kila jambo katika haya lenye kuhusika ki-pekee limeharamishwa - kwahiyo kuchora picha za watu imeharamishwa, na kujenga makaburi ndani ya misikiti imeharamishwa kama yalivyothibitisha maandiko mengine na katika kuyataja baadhi nyengine itakayofuata. Akasema, "Na mapicha yaliyokuwa ndani ya Kanisa ambayo yaliyotajwa na Umm Habibah na Umm Salamah yalikuwa kwenye kuta za Kanisa na mfano wake, hayakuwa na vivuli, kwahiyo kuchora picha zenye kufanana na Mitume na watu wema kwa min-ajil ya kupata baraka na kuponya watu kutokamana nazo ni jambo lililokatazwa katika Dini ya Uislamu na ni 'Ibaada ya masanamu bila ya shaka yoyote. Na Mtume (صلى الله عليه وسلم) ametujulisha yakwamba watu wenye kuchora mapicha hayo ndio hao watakaokuwa miongoni mwa viumbe waovu zaidi mbele ya Allaah katika Siku ya Kufufuliwa.

Uchoraji wa [viumbe walio hai] kwa kutafuta tumbuizo kutokana na kuangalia tu au kwa kujifurahisha na kwa ajili ya kustarehe imeharamishwa na ni katika madhambi makubwa na mwenye kufanya hivyo atakuwa ni miongoni mwa atakaepata adhabu kali Siku ya Kiyama. Kwani yeye ni *Dhaalim*, anaejaribu kuiga vitendo vya Allaah ambavyo hapana asiyekuwa Yeye ndiye awezae kufanya, na hapana anaefanana Nae (سبحانه وتعالى) si kwa dhati Yake, wala si kwa Sifa Zake, wala si kwa vitendo Vyake ameepukana mbali mno na kila sifa za upungufu, Naye ndiye aliye Juu zaidi." Ameyataja haya katika *al-Kawaakib ad-Daraari* (Vol. 2/28/65).

Mimi nasema: "Na wala hapana tafauti baina ya picha zilizochorwa kwa mikono na vyombo vyenye kutumika katika ku-tengeza picha au picha za kamera. Bali, kutafautisha baina ya hizo picha ni ukaidi ulioko katika zama hizi zetu na uhuru wa kujifanyia tutakavyo, kama nilivyoyabain-isha hayo katika kitabu change *Aadaab-uz-Zafaaf* (Uk. 106-116 ya chapa ya pili).

HADEETH: Imepokewa kutoka kwa Jundub ibn Abdullaah al-Bajalee yak-wamba alimsikiya Mtume (صلى الله عليه وسلم), akisema siku tano kabla ya kufa kwake, *"Kwa hakika mimi nilikuwa na ndugu na marafiki miongoni mwenu. [Lakini] kwa hakika niliomba hifadha kutoka kwa Allaah, yakwamba ani-ja'alie niwe na rafiki wa dhati [khaleel] anaetokamana na nyinyi. Allaah (سبحانه وتعالى) amenifanya mimi kuwa ni rafiki wake wa dhati kama Alivyomfanya Ibraahim kuwa ni rafiki yake wa dhati. Na lau kama ningelimchagua rafiki yangu wa dhati kutoka katika Taifa langu, ningelimfanya Abu Bakr kuwa ni rafiki yangu wa dhati. Kwa hakika wale waliokuwa kabla yenu [walikuwa na mazoea] ya kuyafanya makaburi ya Mitume wao na watu wao wema kuwa ni sehemu za kufanyia 'Ibaada. Kwa hakika, musiyafanye makaburi kuwa ni kama sehemu za kufanya 'Ibaada [misikiti]. Mimi nawakataza musifanye hivyo."*

HADEETH: Imepokewa kutoka kwa Haarith an-Najraani aliyesema, "Mimi nilimsikiya Mtume (صلى الله عليه وسلم), siku tano kabla ya kufa kwake akisema: *"Na kwa hakika waliokuwepo kabla yenu walikuwa wakiyafanya makaburi ya Mitume wao na watu wema kuwa ni sehemu zao za 'Ibaada. Mimi nawakataza musifanye hivyo."*

HADEETH: Imepokewa kutoka kwa Usaamah Ibn Zayd yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema alipokuwa akiugua maradhi aliyokufia nayo, *"Waambieni Maswahaba zangu waje kwangu."* Basi wakaingia ndani ya [chumba] alichokuwemo, na hapo alikuwa amefunikwa kwa kitambara cha *'Mu'aafari* cha ki-Yemen . [Basi akajifungua uso wake] akasema: *"Laana ya Allaah iwashukie Mahayudi [na Manaswara]! Wameyafanya makaburi ya Mitume yao kuwa ni sehemu za kufanyia 'Ibaada [masaajid].*

MAELEZO: Nguo hiyo ilikuwa ni ya kutoka Yemen na ilikuwa ikiitwa *Mu'aafari* baada ya kabila la Mu'aafar llililokuwa likihusiana nayo [an-Nihaaya].

HADEETH: Imepokewa kutoka kwa Abu 'Ubaidah Ibn al-Jarraah aliyesema: "Jambo la mwisho ambalo Mtume (صلى الله عليه وسلم) alilolisema lilikuwa ni, *"Wafukuzeni Mayahudi katika ardhi ya Hijaaz na watu wa kutoka Najraan kutoka katika sehemu za Guba la Uarabuni. Na mujue yakwamba miongoni mwa watu waovu*

mno, ni wale walioyafanya [na katika riwaya nyengine inasema: *'... wenye kuyafanya*] *makaburi ya Mitume yao kuwa ni sehemu za kufanyia 'Ibaada [masaajid].*

MAELEZO: Na tafauti katika maana ya matamshi hayo mawili iko wazi. Riwaya ya kwanza imewahusu watu waliopita, nao ni Mayahudi nan Manaswara, kama ilivyokuja kwenye hadeeth zilizotangulia hapo awali. Na